



TANGAZO LA UZABUNI HUDUMA YA CHAKULA

Chuo Kikuu Katoliki Mbeya (CUoM) kinatangaza zabuni ya huduma ya chakula cha wafanyakazi (Kampasi Kuu na New Forest) na wanachuo kampasi ya New Forest kwa mwaka wa masomo 2024/2025. Waombaji wanatakiwa kutimiza vigezo vifuatavyo

A. Vigezo kwa mwombaji

- Kuwa tayari kufanya kazi katika eneo ambalo chuo kitampangia kwa matumizi ya huduma ya chakula.
- Awe tayari kuthibitisha uwezo alionao kifedha kuendesha shughuli anayoomba kwa kuleta taarifa zake za kibenki (bank statement) za miezi mitatu ya mwisho
- Awe na leseni halali ya biashara ya huduma ya chakula
- Awe na uzoefu usiopungua miaka miwili wa kutoa huduma katika zabuni ya chakula
- Mshiriki wa zabuni anapaswa kununua nyaraka za uzabuni (tender document) kuanzia tarehe 04/03/2025 hadi 11/03/2025 saa 4:00 asubuhi hadi 10:00 jioni kwa gharama ya Tsh. 100,000/= Malipo yafanyike katika benki ya CRDB akaunti namba 0150421194101 na risiti ipelekwe ofisi ya uhasibu ili kupata nyaraka za uzabuni.
- Muombaji anapaswa kuainisha kwenye maombi iwapo atapenda kuchukua zabuni ya huduma ya chakula cha wafanyakazi pekee (Kampasi Kuu na/au New Forest), wanafunzi au zote kwa Pamoja.
- Awe na cheti toka mamlaka ya udhibiti na ubora (TBS) au inayohusika na chakula
- Awe tayari kuthibitisha uwezo wa kitaaluma wa kutoa huduma ya chakula

B. Utaratibu wa kurejesha nyaraka za uzabuni utakuwa kama ifuatavyo:

- Nyaraka za uzabuni zirejeshwe katika ofisi ya DVCAF zikiwa zimefungwa na kuandikwa zabuni ya huduma ya chakula kabla ya tarehe 10/03/2025 saa 10:00 jioni. Maombi yatakayofika baada ya muda huo hayatapokelewa
- Maombi ya zabuni yatafunguliwa tarehe 14/03/2025 saa 6:00 mchana katika ukumbi wa mikutano Academic Block, mbele ya waombaji wote.
- Chuo kitamtaarifu mzabuni aliyeshindwa kwa maandishi na hakibanwi kutoa zabuni kwa mshindani aliyetoa bei ya chini. Pia chuo hakitawajibika kutoa sababu kwa wale watakaoshindwa kupata zabuni.